

06-Aina Za Usomaji Wa Qur-aan

Kukithirisha kuisoma Qur-aan ni jambo linalopendeza na kuhimizwa kwa Muislamu ili aweze kufikia kuwa na moyo wenye uhai kwa kufaidika na hayo anayoyasoma kutoka katika kitabu cha Allaah (سبحانه وتعالى). Lengo kubwa katika kuisoma Qur-aan ni kufaidika nayo, na mtu hatoweza kufaidika nayo kama hatokuwa anaisoma kwa kuipa kila herufi haki yake kama walivyopendekeza *maqurraa* wa Qur-aan kulingana na vile walivyopokea; na katika walivyopokea na kuyapendekeza ni aina au daraja tatu zifuatazo:

1- التَّحْقِيقُ At-Tahqiq

Kuisoma polepole sana kwa umakini, kusimama panapopasa kusimama, kuendelea panapopasa kuendelea, kuzingatia maana, kufuata hukmu za Tajwiyd zote, kuipa kila herufi haki yake kutokana na *makhraj* yake, *swiffah* yake, kurefusha herufi za madd zinazopasa kwa hesabu ya juu kabisa katika hukmu yake ya *madd*, kutokurefusha zisizopasa kurefushwa, kuzitamka herufi za التَّفخِيمِ و التَّرْقِيقِ (*at-tafkhiym wa tarqiyq* – nzito na nyepesi) kama ipasavyo. *Qiraa-ah* hiki husomwa zaidi na Mashaykh (hususan) kwa lengo la kurekodi, kuwafunza wanaoanza kujifunza kusoma Qur-aan.

2- الحَدْر Al-Hadr

Kusoma Qur-aan kwa mwendo haraka haraka, huku ukifuata masharti yote ya usomaji sahihi wa hukmu za Tajwiyd. Kwenye *madd* za kuchagua hesabu za *harakaat*, msomaji huvuta kwa hesabu ya chini. Msomaji awe na tahadhari kutokufupisha herufi za *maddul-laazim*. Kutokuacha kufanya *ghunnah*, *ikhfaa*, kudhihirisha herufi, pamoja na kufuata hukmu zote za kupumzika na kusimama.

التدوير - 3 At-Tadwiyr

Kusoma Qur-aan kwa (daraja ya) wastani baina ya viraa viwili vya *At-Tahqiq* na *Al-Hadr* huku ukifuata hukmu za Tajwiyd . Kisomo hiki ndicho cha kawaida na kinachotumika sana.

Hizo ndizo aina au daraja za usomaji wa Qur-aan na zinaruhusiwa kwa manufaa na sharti kuwa msomaji anaweza kuchagua kile kilicho *munaasib* kwake maadamu ataweza kufaidika na kile anachokisoma; kwani vyote vinajumuika katika neno la '*tartiyl*' kama ilivyotajwa katika Qur-aan:

﴿ وَرَتِّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلاً ﴾

((na soma Qur-aan kwa *tartiylaa* [kisomo cha utaratibu upasao]))¹

Utaona visomo vyote tulivyovitaja vinahitaji kuchunga hukmu za Tajwiyd na kuchunga makosa bila kuchanganya maneno wala herufi. Ama visomo vya haraka vinavyosomwa na baadhi ili tu wamalize haraka huku wakiyakata maneno na kuchanganya herufi viko mbali na makusudio ya aina za visomo ambavyo Muislamu anafaidika navyo na kupata malipo mbele ya Allaah (سبحانه وتعالى). Mfano ni pale watu wanapokusanyika kwa madai ya kukhitimisha Qur-aan; watu hugawa misahafu au juzuu na kuanza mashindano ya usomaji wa kasi huku hawana habari na wanachokisoma. Pia katika mwezi Ramadhaan ambapo Waislamu wanajitahidi kumaliza Qur-aan, mara kadhaa utawakuta wengi wanasoma kwa kasi mno bila ya kuchunga hukmu za Tajwiyd .

¹Al-Muzzammil (73: 4)